

HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA

MTIHANI WA KUJISOMEA NYUMBANI KWA DARASA LA SABA 2020

SOMO: KISWAHILI

MUDA: SAA 1:30

JUNI 2020,

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A,B,C,D na E zenye jumla ya maswali **arobaini na tano (45)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
4. Andika **jina lako, shule na somo kwa usahihi katika karatasi yako ya kujibia.**

SEHEMU A: SARUFI

Chagua herufi ya jibu sahihi kisha siliba herufi ya jibu hilo katika karatasi maalumu ya kujibia uliyopewa.

1. Yule msichana anaimba vizuri, neno **msichana** limetumika kama aina ipi ya maneno?
a) Nomino
b) Kitenzi
c) Kielezi
d) Kivumishi
e) Kiwakilishi
2. Hakuna ruhusa mnyamakuingia katika mazingira ya shule
a) Yeyote
b) Wowote
c) Yoyote
d) Popote
e) Chochote
3. Shangazi anapika vizuri. Hii ni aina ipi ya sentensi?
a) Changamano
b) Shuruti
c) Sahili
d) Tata
e) Ambatano
4. Kutokuwa na subra kulimfanya Juma aache kazi, neno **subra** limetumika kama.....
a) Kielezi
b) Kivumishi
c) Nomino
d) Kielezi
e) Kitenzi
5. Nilipokwenda nyumbani kwao
a) Nikamkuta
b) Sijamkuta
c) Nikakuta
d) Sikumkuta
e) Sikumkutaga
hayupo
hayupo
6. Kitasa kimevunjwa na Asha, sentensi hii ipo katika kauli ipi?
a) Kutenda
b) Kutendewa
c) Kutendana
d) Kutendwa
e) Kutendeka
7. Nomino **Chui** ipo katika ngeli ipi?
a) A-WA
b) U-I
c) KI-VI
d) I-ZI
e) U-YA
8. Neno lipi kati ya haya lina maana karibu sawa na neno **kito**?
a) Fahari
b) Johari
c) Samani
d) Tuzo
e) Zawadi

SEHEMU C: UTUNGAJI

Malizia simu ifuatayo kwa maneno matano tu.

JUMA NGULUNGU SLP 260 MWANZA;Mjulisha kwamba baba yake ni mgonjwa anahitaji msaada wa fedha haraka. Jina lako ni **Mwalima**

31.
32.
33.
34.
35.

SEHEMU D: USHAIRI

1. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali

1. Kuna mnyama mmoja , simfahamu kwa jina
Watu wengu humtaja, lau hawajamwona
Mnyama huyu wa kuja, bado hajajulikana
Mnyama huyu ni yupi, jina lake silijui

2. Ni hodari wa safari, na mizigo kuchukua
Ana nguvu za fahali, hachoki akitembea
Mwenyeji wa Kalahari, Sahara na Arabia
Mnyama huyu ni yupi, jina lake silijui

36. Kichwa cha shairi hili kinafaa kuwa.....

- a) Mnyama nisiyemjua d) Kitendawili
b) Simjui huyu mnyama e) Anaitwa nani?
c) Mnyama ninayemtaja

37. Katika ubeti wa kwanza, mshairi anasema **mnyama huyu wa kuja** akimaanisha kuwa

- a) Si wa asili hapa kwetu d) Hana thamani
b) Ni mzee e) Anajulikana sana hapa kwetu
c) Ni mtalii

38. Sentensi ipi siyo ya kweli kuusu mnyama anayesemwa?

- a) Ananyonyesha ndama c) Anabeba mizigo mizito
b) Nyama yake inaliwa d) Ana mbio kama za Twiga

e) Anamudu kutembea kwenye mchanga

39. Kitu kinachomwezesha mnyama huyu asizame kwenye mchanga ni.....

a) Uzito wake mdogo

d) Maarifa aliyonayo

b) Mbio zake ndefu

e) Ngozi nyembamba kwenye kwato

c) Umbile lake la kichwa

40. Mnyama anayetajwa katika shairi hili ni yupi?

a) Tembo

c) Farasi

e) Punda

b) Ngamia

d) Twiga

SEHEMU E: UFAHAMU

Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali

Ni jambo la ujinga kuchagua fedha na kuiweka awali kama chombo cha maendeleo. Hali twajua nchi yetu ni duni. Ni ujinga vilevile tukiikazania dhania hiyo ya unyonge wetu kwa kuitegemea fedha kutoka nchi ya **ughaibuni** badala ya fedha zetu wenyewe. Ni ujinga kwa sababu mbili, kwanza hatuwezi kuzipata ingawa ziko nchi zenye neema zinazoweza kutoa misaada na mikopo, lakini bado misaada hiyo na mikopo hiyo haitoshi kwa nchi changa kama Tanzania.

Kama twataka maendeleo hatuna budi kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa, misaada yaweza kuhatarisha usalama wan chi.

MASWALI

41. Neno **duni** kama lilivyotumika katika habari lina maana gani?

.....

42. Ughaibuni katika habari lina maana gani?

.....

43. Ili tuepuke mikopo yatubidi kufanyaje?

.....

44. Mwandishi anasema zipo nchi zenye neema zinazoweza kutoa kitu gani?

.....

45. Kichwa cha habari hii kinafaa kiitwe'

.....